## Tabuleti ya Najuta



Najuta alinunuliwa tabuleti na wazazi wake. Walikusudia kuwa kifaa hicho kingemsaidia Najuta katika masomo yake. Maskini wazazi wa Najuta hawakujua kuwa kifaa hicho kingekuwa chanzo cha masaibu yao!

Najuta aliifungua tovuti iliyomsisimua sana siku moja. Ghafla, ujumbe mfupi ulichipuka. Najuta aliarifiwa kuwa amebahatika kupata nafasi ya kuhudhuria karamu ya kukata na shoka kijijini. Alionywa kwamba angemjuza yeyote kuhusu bahati yake, ingemponyoka. Alitarajiwa kufika katika kituo cha mabasi ya kuelekea jijini mapema siku iliyofuata.

Hauchi hauchi unakucha! Najuta alifika kwenye kituo cha mabasi kama alivyokuwa ameelekezwa. Mwanamke aliyekuwa amevaa nguo nadhifu alimuita kwa jina kisha akamsalimia. Alimkaribisha katika gari la kifahari lililokuwa limeegeshwa hapo karibu.

Maskini Najuta hakumbuki kilichotokea! Alijipata katika chumba fulani. Muda mfupi baadaye, mwanamume aliyetisha kama mauti aliingia chumbani humo. Alimpokeza Najuta rununu na kumfokea awapigie wazazi wake simu.

Najuta aliipiga simu huku akilia. Upande wa pili aliisikia sauti ya mama yake. Ghafla, mwanamume yule alimpokonya simu ile. Alimweleza mamake Najuta kwamba mwana wao angekuwa mashakani asingezituma shilingi milioni moja kupitia nambari iliyotumika kumpigia simu. Mwanamume huyo aliikata simu na akaondoka chumbani.

Muda mchache baadaye, Najuta alizisikia kelele nje ya chumba. Kumbe maafisa wa usalama walikuwa wakiifuata mienendo ya watekaji nyara! Hiyo ilikuwa siku yao ya arubaini.

Najuta aliokolewa na kurudishwa kwao. Wahalifu hao walitiwa mbaroni na sheria ikaufuata mkondo wake. Najuta alijua umuhimu wa kuzifuata hatua za usalama wakati wa kusakura mtandaoni.